# STD 5 END TERM 3 EXAM 2019

## KIWAHILI

Muda: Saa 1 dakika 40

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

Bidhaa __1__ katika duka __2__ ni __3__. Baba __4__ hununua kwa jumla na kuzigawanya kwenye __5__ ambazo huwekwa juu ya __6__. Linafunguliwa alfajiri __7__ ya jua kuchomoza kutoka __8__. Wakati __9__ wateja __10__ wengi kama adhuhuri. Baba husema kuwa familia __11__ kuepuka kutumia pesa __12__. La __13__ biashara itaanguka na mahitaji __14__ yatakosekana. Kwa hakika tuna duka __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. zilizo | B. vilivyo | C. iliyo | D. yaliyo |
| **2.** | A. wetu | B. yetu | C. zetu | D. letu |
| **3.** | A. ndogo ndogo | B. madogo madogo | C. vidogo vidogo | D. dogo dogo |
| **4.** | A. letu | B. zangu | C. wangu | D. yetu |
| **5.** | A. makaratasi | B. karatasi | C. makartasi | D. kartasi |
| **6.** | A. paa | B. rafu | C. kabati | D. dari |
| **7.** | A. badala | B. mbele | C. kabla | D. baada |
| **8.** | A. mashariki | B. kusini | C. magharibi | D. kaskazini |
| **9.** | A. hizo | B. huo | C. hiyo | D. huwo |
| **10.** | A. hawi | B. hawakui | C. hawawi | D. hawakuwi |
| **11.** | A. anafaa | B. wanafaa | C. unafaa | D. inafaa |
| **12.** | A. nzuri | B. vizuri | C. vibaya | D. mbaya |
| **13.** | A. sivyo | B. katakata | C. hasha | D. siyo |
| **14.** | A. mingi | B. mengi | C. nyingi | D. mwingi |
| **15.** | A. kibora | B. libora | C. mbora | D. bora |

***Kutoka swali la 16-30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. **Andika kinyume cha:**
Mwalimu amefika asubuhi.
A. Mwanafunzi ameondoka jioni.
B. Mwalimu atafika mchana.
C. Mwalimu mkuu ameenda jioni.
D. Mwanafunzi ameondoka asubuhi.

17. Msumari ulianguka sakafuni ______!
A. pu B. ti
C. tang D. chubwi

18. **Kamilisha methali:** Paka akitoka
A. raha kwa panya
B. hurudi
C. panya huingia
D. panya hutawala.

19. Mahindi yakisagwa hutoa unga
A. jeupe B. weupe
C. mweupe D. nyeupe.

20. Chagua sentensi iliyotumia **'-o-ote'** vizuri.
A. Usiweke tu nyasi yoyote kwenye nyumba.
B. Kipepeo yeyote huwapendeza watalii.
C. Nitavaa nguo lolote nikienda shambani.
D. Msimkaribie mnyama wowote mbugani.

21. Mmea unaozaa pareto huitwa
A. mbuni B. mtunguja
C. mpareto D. mpera.

22. **Kanusha:** Sakafu inapigwa deki.
A. Sakafu haijapigwa deki.
B. Sakafu haipigwi deki.
C. Sakafu haikupigwa deki.
D. Sakafu haitapigwa deki.

23. Randa ni kifaa cha
A. kulainishia mbao
B. kukatia mbao
C. kupimia usawa wa ukuta
D. kutobolea mashimo.

24. Chagua maelezo sahihi.
A. Kipofu ni mtu mwenye jicho moja.
B. Bubu hawezi kuongea.
C. Kiziwi hawezi kusikia wala kuongea.
D. Kiguru ni mtu asiye na mkono mmoja.

25. Chagua neno linalojumlisha mengine yote.
A. Thumni B. Akisami
C. Robo D. Ushuri mbili

26. Sima hupikwa kwa kusongwa ilhali mayai
A. hukarangwa B. huchomwa
C. hukaushwa D. hukaangwa.

27. **Kamilisha sentensi kwa jibu sahihi.**
Mwizi ____ aliachiliwa huru amekamatwa tena.
A. ambazo B. ambae
C. ambao D. ambaye

28. Chagua sentensi iliyoakifishwa vyema.
A. Umemwona musa leo?
B. umemwona musa leo?
C. Umemwona Musa leo?
D. umemwona Musa Leo?

29. Kinda ni mtoto wa
A. simba B. ndege
C. kuku D. ng'ombe.

30. Baba hapendi chai wala uji. Hii inamaanisha
A. baba anapenda chai zaidi
B. baba anapenda uji zaidi
C. baba anapenda vinywaji vyote viwili
D. baba hapendi kinywaji chochote kwa hivi viwili.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.***

Mashindano ya nyimbo na mashairi yalifanyika mwezi wa saba katika shule ya Fanisi. Shule yetu ya Shupaza ilikuwa imejiandaa vilivyo kwa siku hiyo. Mwalimu wetu, Bw. Oke, alikuwa ametunga mashairi matatu. Ilibidi tuyasome na kunakili yote vitabuni kabla ya kufundishwa jinsi ya kuyakariri. Hiyo haikuwa kazi ngumu kwani yalikuwa na mishororo minne minne tu katika kila ubeti.

**Siku ya siku** ilipofika tulishangaa kukuta shule nyingi zikiwa zimefika kushiriki. Ushindani ulikuwa mkali lakini kwa bidii zetu za mchwa, tuliibuka washindi katika mashairi mawili. Kwa kuwa chanda chema huvikwa pete, tulipewa kikombe na kupata nafasi ya kumtumbuiza rais kwenye ikulu yake.

**31.** Mashindano yalifanyika lini?
- A. Muhula wa pili.
- B. Wiki ya saba.
- C. Muhula wa tatu.
- D. Baada ya mwezi wa saba.

**32** Shule ya Fanisi
- A. ilikuwa na mashairi matatu
- B. ilivuta mkia katika mashindano
- C. iliibuka mshindi katika mashairi yake
- D. iliandaa mashindano.

**33.** Kulingana na ufahamu, Bw. Oke alikuwa
- A. mwalimu wa hesabu
- B. malenga
- C. mwimbaji wa mashairi
- D. mwenye shule.

**34.** Kabla ya kufundishwa kukariri mashairi, wanafunzi
- A. waliyaandika na kukariri
- B. walishindana na kutuzwa
- C. waliyasoma na kunakili
- D. walitunga na kuimba.

**35.** Mashairi yenye mishororo minne katika kila ubetu huitwa
- A. tarbia
- B. tathlitha
- C. takhmisa
- D. robo.

**36.** **Siku** ya siku inamaanisha
- A. siku ya mashindano
- B. siku ndefu kabisa
- C. siku ya kujifunza
- D. siku nyingi.

**37.** Mchwa amelinganishwa na sifa gani katika ufahamu?
- A. Bidii
- B. Sauti nyororo
- C. Uzembe
- D. Ukali

**38.** Shule ya Shupaza ilishinda katika
- A. nyimbo tatu
- B. shairi moja tu
- C. mashindano yote
- D. mashairi mawili.

**39.** Walioibuka washindi walipewa nini?
- A. Pesa
- B. Kikombe
- C. Ikulu
- D. Dhahabu

**40.** Chagua methali iliyotajwa kwenye ufahamu.
- A. Mcheza kwao hutuzwa.
- B. Dawa ya moto ni moto.
- C. Chanda chema huvikwa pete.
- D. Lila na fila havitangamani.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.***

Kola alikuwa na tabia ya kukojoa kwenye malazi licha ya kuwa na miaka kumi. Mwalimu alituambia mtu kama huyo huitwa kikojozi. Mama yake hakuipenda tabia hiyo kwa sababu alimwona kama mtu mkubwa. Kila asubuhi angemwamuru kuyatoa malazi yote nje ili harufu mbaya ya mkojo ipungue. Pia yangekauka mchana akiwa shuleni. Mtindo huu wa kuanika na kuanua malazi ulianza kumkera Kola hata akawa anasahau kuyarudisha ndani ya nyumba.

Kwa kuwa uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi, mama yake angeanua malazi ya mwanawe ili alale fofofo. Lakini alipokumbuka kuwa Kola anafaa kukua akijua majukumu yake, aliona heri amfunze adabu. Basi Jumamosi moja Kola alianika malazi na kwenda kucheza na rafikiye alasiri. Kwa bahati mbaya, mvua ilianza kunyesha. Kola alikaa kwa rafikiye akijua kuwa mama angekuwa mama. Lakini mama aliyaacha **yakalowa chepechepe**. Usiku huo Kola hakupata hata lepe la usingizi na ukawa mwisho wa kuwa kikojozi.

**41.** Mtu mwenye tabia ya kukojoa malazini huitwa

A. Kola B. mkojo
C. kikojozi D. kojoa

**42.** Kola alikuwa na miaka mingapi?

A. Saba B. Minane
C. Kumi D. Tisa

**43.** Mama alichukizwa na tabia ya Kola kwa sababu

A. Kola alikojoa kwenye malazi
B. Kola hakupenda kuanika malazi
C. alimwonya kwa muda mrefu
D. alimwona kama mtu mkubwa.

**44.** Malazi yalitolewa nje wakati gani?

A. Jioni
B. Asubuhi
C. Usiku
D. Alasiri.

**45.** Kilichomkera Kola ni

A. kuanika na kuanua malazi
B. kuenda shuleni kila siku
C. kuenda haja ndogo
D. kukemewa na mama.

**46.** Ni nani aliyeanua malazi Kola aliposahau?

A. Mama yake
B. Baba yake
C. Mwalimu wake
D. Rafiki yake.

**47.** Kola alifunzwa adabu kwa

A. kufukuzwa shuleni
B. kuacha malazi yanyeshewe
C. kukatazwa kumtembelea rafikiye
D. kucharazwa viboko.

**48.** Majukumu ni

A. malazi yaliyoloa
B. mambo ambayo mtu anafaa kufanya
C. hali isiyopendeza
D. adhabu.

**49.** **Kulowa chepechepe** ni mfano wa

A. tanakali ya sauti
B. methali
C. tashbihi
D. nahau.

**50.** Ni kweli kuwa Kola

A. anapanga kuacha kukojoa malazini
B. anaendelea kukojoa malazini
C. hakojoi malazini tena
D. hawezi kuacha kukojoa.